JINA---------- NAMBA YAKO.....

SAHIHI YA MTAHINIWA----------

102/2

KISWAHILI KARATASI YA 2

LUGHA

MUDA : SAA 2 ½

JULY/AUGUST 2013

TAREHE: 24/7/2013

SAA: 4.30 – 7.00 Mchana

2013 RABAI DISTRICT MOCK EXAMINATION

Kenya Certificate Of Secondary Education (KCSE)

MAAGIZO

- Hakikisha umeandika jina na nambari yako
- Jibu maswali yote
- Majibu yako yaandikwe katika nafasi zilizoachwa katika kijitabu hiki cha maswali

Kwa matumizi ya mtahiniwa pekee.

Swali	Upeo	Alama
1	15	
2	15	
3	40	
4	10	
Jumla	80	

Karatasi hii ina kurasa 5 zilizopigwa chapa. Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.

1. UFAHAMU

Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali.

Kwa sababu ya bongo alizonazo binadamu ana uwezo wa kutumia teknolojia kwa manufaa yake na ithibithi zipo tele. Binadamu ametumia nyambizi kuzuru chini ya bahari, amefika mwezini, amevumbua magala,amevumbua uyoka, amevumbua tarakilishi na shughuli zake ni kutandaridhi. Mwenyewe yuasema kuwa dunia yake imekuwa kitongoji katika muumano huu.

Chambilecho wavyele, akili huondoa maarifa. Binadamu amekuwa dumbwana linalijenga koshoto na kuibomoa kulia na tuna sababu ya kulisoza dubwana hili kidole. Rabana ndiye msanii asiye mfanano kwani aliisawiri muruwa. Rabuka akaona yote yaliyokuwa mema na mazuri akamwambia binadamu, 'Haya twende kazi!'

Viwanda vya binadamu vinatiririsha maji-taka ovyo hadi mtoni, maziwani na baharini na matokeo yamekuwa ni vifo vya viumbe vya majini kama samaki ambavyo ni uriothi aliopewa na Muumba. Hakuna kiumbe kinachoweza kustahimili maisha bila maji safi. Maji hayo sasa yametiwa simu na binadamu kwa sababu ya maendeleo yake. Moshi kutoka katika viwanda vivyo hivyo nao umehasiri ukanda wa ozone ambao sasa umeruhusu jua kutahasiri kwa joto kali mno . Siku hizi inasemekana kuwa kuna mvua ya asidi inayonyesha katika baadhi ya sehemu za dunia na kuleta maradhi makubwa. Labda hata mabahari yamekasirika kwa sababu ya yale yanayofanywa na binadamu. Labda hata mabahari yamekasirika kwa sababu ya yale yanayofanywa na binadamu. Vimbunga navyo vimetokea kwa wingi wataalamu wanasema kuwa viwango vya myeyuko vitazidi kwa sababu ya joto na kiwango cha maji kitazidi pia. Binadamu atatorokea wapi?

Idadi ya binadamu imezidi hadi kiwango asichoweza kukishughulikia kwa sababu anaijaza kiholela kwa sababu anadai kuwa aliruhusiwa kuijaza.Hii ni imani potovu. Anasahau kuwa alipewa ubongo wa kuwaza na kuwazua kabla ya kufanya chochote . Dhaka, maradhi na ufukara vimehamia kwa binadamu na kumtia kiwewe.

Binadamu amefyeka misitu kwa kutaka makao, mashamba , mbao makaa, ujenzi wa nyumba, barabara na mahitaji mengi. Wanyama wamefurushwa na wengi kuangamia kwa sababu ya ukosefu wa chakula na wengi kushindwa kuhimili mabadiliko katika mazingira. Chemichemi za maji zimekauka nalo jangwa limeanza kutuzuru kwa kiasi inayotisha. Kazi ya binadamu imekuwa ya kusukia kamba motoni.

MASWALI

a) NI mambo gani yamechangia kuifanya dunia kuwa kitongoji? (ala 1)

……

……

b) Ni sababu gani zinazomfanya binadamu kuwa dubwana? (ala 2)

……

……

c) Kwa kurejelea taarifa, dondoa madhara yanayotokana na viwanda. (ala. 4)

……

……

……

……

d) Kwa mujibu wa habari hii, eleza itikadi za binadamu. (ala. 2)

……

……

……

……

e) Kwa kurejelea habari fafanua madhara yanayotokana na ukataji wa miti kiholela.(al.3)

……

……

……

……

f) Eleza maana ya vifungu kama vilivyotumiwa katika taarifa hii. (ala. 3)

i) Kutandaridhi

……

……

ii) Maji-taka

……

……

iii) Kusukia kamba motoni

……

……

2. **UFUPISHO**

Aina Fulani ya kansa huwapata zaidi wanaume. Kansa ya tezi-kibodfu, ya koromeo na ya mapafu ni baadhi ya hizo. Kansa ya tezi- kibofu huwalenga sana wazee wa umri wa miaka sitini na zaidi. Je umejiuliza sababu ya kina babu kuenda haja ndogo mara kwa mara? Hii ni dalili mojawapo ya kansa. Zingine ni ugumu wa kupitisha mkojo. Kuanza kutoa damu kwenye mkojo, maumivu ya mgongo na kadhalika. Mwisho tezi- kibofu huzidi kwa ukubwa na kufunga mkojo kutoka.

Kansa zinazowapata zaidi wanawake ni: ya nyumba ya uzazi, ya mlango wa uzazi na maziwa. Kansa ya maziwa inatisha mno. Wanawake wenye umri wa miaka thelatini na mitano na zaidi wamo hatarini kuliko wote. Dalili za awali ni uvimbe unaohisika kwa ndani, na maziwa kutoa usaha, Kansa ya maziwa huenea upesi na huviambukiza viungo vilivyo karibu kama vile mapafu, ini na kadhalika.

Madaktari wanapendekeza mambo kadhaa. Kwanza ni ukaguzi wa kibinafsi kwenye viungo vilivyo na uwezekano mkubwa wa kuambukizwa. Kisha jambo lolote lisilo la kawaida kama uvimbe, ugumu wa kumeza na kadhalika mara moja kwa daktari. Daktari atafanya uchunguzi wake na kuamua ni lipi linaoimfaa mhusika.

Kadhalika, ushauri zaidi ni kuhusu aina ya vyakula na mitindo ya kisasa ya maisha . Vyakula vilivyojaa protini zinazopatikana katika nyama na mayai ni miongoni mwa vyakula hatari. Mafuta kutokana na mimea hupendekezwa. Uvutaji wa sigara, unywaji wa pombe na baadhi ya vipodozi vya kisasa vyenye zebaki huweza kuzidisha uwezekano wa kupata kansa. Tukizingatia masharti haya, tutaziba ufa na kujiepusha na kujenga ukuta.

Saratani ni kama sikio la kufa ambalo halisikii dawa. Ikigunduliwa mapema, matibabu huanzishwa kwa kutumia dawa, tibakemikali, tiba ya miale ambayo huzichoma kwa miale chembechembe zilizoambukizwa.

Ikizidi lisilobudi hutendwa. Huwa hakuna budi kuingo kuondolewa kwa upasuaji ili kuokoa sehemu zingine na maisha kwa ujumla. Kwani wahenga hawakushauri, ‘ kata pua uunge wajihi?’

MASWALI

a) Fupisha aya tatu za kwanza kwa maneno kati ya 60 – 65

(alama 9, utiririko 2)

Matayarisho

……..

……..

……..

……..

……..

……

Jibu

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

b) Eleza njia ambazo zinaweza kutimiwa kuzuia na kutibu saratani. (maneno 45-50)
(alama 6 utiririko 1)

Matayarisho

……

……

……

……

……

……

Jibu

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

2. MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)

a) Eleza tofauti na mfanano uliopo baina ya sauti /f/ na /v/ (alama 2)

……

……

b)Huku ukitoa mifano eleza maana ya kiimbo. (alama 2)

……

……

c) Tambua ni hali gani inayowasilishwa katika sentensi hii.
Osama auawa. (alama 1)

……

……

d) Bainisha matumizi ya “kwa’ katika sentensi ifuatayo.
Omar alikwenda Nairobi kwa ndenge kusheherekea kwa shangwe kufaulu kwake alipopata tisini kwa mia. (alama 2)

……

……

e) Andika sentensi ifuatayo katika ukubwa

Watoto walilemewa na uzito wa vitabu. (alama 2)

……

……

f) Bainisha shamirisho katika sentensi hii

Nilimnunulia mwanangu kitabu kwa marupurupu niliyopata. (alama 3)

……

……

……

……

g) Andika sentensi hii upya ukitumia ‘o’ rejeshi tamati.
Zimwi ambalo humla mtu ni lile ambalo linaogopewa. (alama 2)

……

……

……

……

h) Kanusha sentensi ifuatayo.
Mpishi amepika chai pia na chakula. (alama 2)

……

……

……

i) Sahihisha sentensi ifuatayo'
Nilipopinduka nyuma niliona na macho manyumba yota yanateketea. (alama 2)

……..

……..

……..

j) Andika sentensi ifuatayo katika wakati ujao hali timilifu.
Bebora alinunua pikipiki. (alama 2)

……..

……..

……..

……

K) i) Taja vipashio ulivyotoa hapo juu. (alama 2)

……..

……..

……..

……

II) mifani miwili ya vipashio ulivyotoa hapo juu (alama 2)

……..

……..

……..

……

l. Bainisha viambishi awali na tamati katika neno
mnagombeana. (alama 2)

……..

……..

……..

m. Tunga sentensi katika wingi ukitumia maneno yaliyo katika mabano ili yalete dhana zifuatazo. (alama 2)

i) Amri (pa)

……

……

……

ii) Swali (ja)

……

……

……

n. Changanua sentensi ifuatayo kwa kutumia matawi.
Mtu wao aliyepotea ufuoni ingawa hakuwa na nguo. (alama 4)

……

……

……

……

o. Ainisha maneno katika sentensi hii.
Wawili waliangua kicheko garini. (alama 2)

……

……

……

p. Bainisha aina za vielezi katika sentensi hii.
Alibebwa hobelahobela huku akichapwa kama mbwa hadi kwenye gari. (alama 2)

……

……

……

q) Andika sentensi ifuatayo katika usemi halisi
Mwalimu Mkuu alisema kwamba wote waliorudi shuleni kuchelewa wangefanya mtihani mwingine kwa kuwa wenzao walikuwa wamemaliza kufanya mtihani siku mbili zilizopita.. (alama 2)

……..

……..

……..

r. Andika kinyume cha neno lililopigwa mstari.
Kamau amehama mjini. (alama 1)

……..

……..

ISIMU JAMII (ALAMA 10)

Jadili hatua muhimu za historia na kukua kwa Kiswahili nchini Kenya kuanzia wakati wa uhuru hadi sasa.

……..

……..

……..

……

……..

……..

……..

……

……..

……..

……..

……

……..

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

ANSWERS:

Order a copy of answers from www.schoolsnetkenya.com/order-e-copy

NB> We charge Kshs. 100 ONLY to meet website, e-resource compilation and provision costs